

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

04

HISABATI



Muda: Saa 1: 30

Mwaka: 2019

Maelekezo

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**
3. Kila swali lina **alama (10)**

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
1.	(a)	Andika tarakimu ya maelfu, mamia, makumi na mamoja katika namba 10,529 kwa maneno..		
	(b)	Andika 49 kwa namba za Kirumi.		
	(c)	Je, tarakimu ipi katika namba 78,421 ipo kwenye makumi elfu?		
	(d)	Andika namba ifuatayo kwa kifupi: 8000 + 400 + 60 + 3.		
	(e)	Kitabu kina kurasa mia tatu na nane. Andika kurasa za kitabu hiki kwa numerali..		
2.	(a)	Andika namba inayofuata katika mpangilio wa namba zifuatazo: 4,6,8,10, _____.		
	(b)	Panga namba zifuatazo kwa mpangilio unaoanza na namba ndogo hadi namba kubwa zaidi: 9, 3, 11, 5, 7, 1, 13.		
	(c)	Andika namba zinazokosekana katika mpangilio wa namba za kirumi: X, XV, XX, _____, XXX, _____.		
	(d)	Jaza namba iliyokosekana katika mpangilio wa namba: 461, 361, 261, _____ 61.		
	(e)	Mfanyabiashara alinunua machungwa 64, mapapai 42, maembe 100 na ndizi 98. Panga majina ya matunda hayo kwa kufuata idadi yake kuanzia mengi hadi machache zaidi.		

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
3.	(a)	Jumlisha; $1,564 + 315 =$		
	(b)	Gawanya; $15)900$		
	(c)	Kitabu kina kurasa 91, ikiwa kila ukurasa una picha 13 tafuta jumla ya picha zilizomo ndani ya kitabu hicho.		
	(d)	Zidisha; $72 \times 58 =$		
	(e)	Idadi ya pundamilia katika hifadhi moja ya Tanzania ilikuwa 3,211. Iwapo waliongezeka pundamilia 195 mwaka uliofuata tafuta jumla ya pundamilia katika hifadhi hiyo.		
4.	(a)	Andika jina la mstari ufuatao : 		
	(b)	Ni sehemu gani ya umbo lifuatatalo limewekewa kivuli? 		

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
	(c)	<p>Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo:</p> 		
	(d)	Bustani ya Jamila ina umbo la pembetatu. Upande wa kwanza una urefu wa m 10, wa pili m 25 na wa tatu m 18. Tafuta mzingo wa bustani hiyo.		
	(e)	Mzingo wa mstatili ni sm 42. Ikiwa urefu wake ni sm 12, tafuta upana wa mstatili huo.		
5.	(a)	<p>Jumlisha;</p> $\text{Sh. } 2,570 + \text{Sh. } 1,650 =$		
	(b)	<p>Toa;</p> $\text{Sh. } 2,780 - \text{sh. } 1,890 =$		
	(c)	<p>Zidisha;</p> $ \begin{array}{r} \text{Sh. } 2\ 0\ 0 \\ \times\ 2\ 5 \\ \hline \end{array} $		

Na.	Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
(d)	Kalunde alimpa bibi yake shilingi elfu kumi na tano. Pia Sara alimpa bibi yake elfu tano. Je, bibi alipokea jumla shilingi ngapi?		
(e)	Meza moja inauzwa sh. 7,000. Je, meza tano zitauzwa shilingi ngapi?		